

**MATUKIO YA UZINDUZI WA WIKI YA CHANJO
SAMBAMBA NA UWEKAJI WA JIWE LA MSINGI ZAHANATI
YA ISOMIA 24/4/2023 KATIKA PICHA**



Mkuu wa Wilaya ya Singida mhansisi Paskas Muragili, akizindua wiki ya chanjo kitaifa kwa kuitoa chanjo kwa mmoja wa watoto wenye umri chini ya miaka mitano ambao hawakupata chanjo tangu kuzaliwa pamoja na chanjo ya kuzuia saratani ya mlango wa kizazi kwa mabinti wenye umri kuanzia miaka 9 hadi 14 .



Mkuu wa Wilaya wa Singida Mhandisi Paskas Muragili akipongezwa baada ya kuweka jiwe la msingi katika mradi wa ujenzi wa zahanati ya Mtaa wa Isomia. Shughuli hii ni miongoni mwa shuguli zinazotekelezwa katika kuelekea kilele cha maadhimisho ya miaka 59 ya muungano wa Tanganyika na Zanzibar tarehe 26/4/2023. Kushoto ni Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa Bi. Upendo Naftali na kulia ni Diwani Kata ya Mwankoko Mhe. Emmanuel Emadaki



Mkuu wa wilaya Mhandisi Paskasi Mragili akitoa maelekezo baada ya kukagua mradi wa ujenzi wa zahanati ya Isomia



Mgeni Rasmi, Mkuu wa wilaya ya Singida akiongoza wananchi na viongozi mbalimbali katika zoezi la upandaji miti katika eneo mradi wa zahanati, zaidi ya miti 60 imepandwa.



Bi. Upendo Naftali, Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii wa Manispaa, aliyemwakilisha Mkurugenzi katika uzinduzi wa wiki ya chanjo na uwekaji wa jiwe la msingi zahanati ya Isomia, akipanda mti katika eneo la zahanati hiyo



Mratibu wa chanjo Manispaa ya Singida, Bi. Digna Sakaya (Kushoto) akisimamia zoezi hilo baada ya uzinduzi kukafnyika katika eneo la mradi wa ujenzi wa Zahanati ya Isomia. Mgeni Rasmi, Mkuu wa Wilaya ya Singida Mhandisi Paskas Muragili ametoa agizo kwa mganga Mkuu wa Manispaa kuhakikisha huduma za kliniki za watoto na wanawake wajawazito zinatolewa kila wiki kutokana na umbali uliopo wa kilometa 6 kutoka Isomia mpaka zahanati ya Mwankoko



Baadhi ya wananchi waliojitokeza katika shughuli ya uzinduzi wa wiki ya chanjo kitaifa pamoja na uwekaji wa jiwe la msingi katika zahanati ya Isomia ikiwa ni mwendelezo wa shughuli mbalimbali zinazofanyika kuelekea kilele cha maadhimisho ya mika 59 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.



Diwani wa Kata ya Mwankoko, Mhe Emmanuel Emadaki, akifuatiwa na Mtendaji wa Kata ya Mwankoko Bi. Habiba Juma, wakiungana na wananchi kucheza ngoma ya asili ya kabila la kinyaturu wakati wa uzinduzi wa wiki ya chanjo kitaifa pamoja na uwekaji wa jiwe la msingi katika zahanati ya Isomia